

Je, ninapaswa kufanya nini ikiwa nimebainishwa kuwa na ugonjwa? **HOMA YA NYANI (MONKEYPOX)**

Nimeambiwa kwamba ama nina kisa kinachowezekana au kilichothibitishwa cha homa ya nyani, ninahitaji kujua nini?

MATIBABU YA HOMA YA NYANI

Hakuna matibabu mahususi ya maambukizi ya homa ya nyani, hata hivyo, virusi vya homa ya nyani na ndui vinafanana kijenetiki, jambo linalomaanisha kwamba dawa za kuua virusi zilizoundwa ili kutoa ulinzi dhidi ya ndui zinaweza kutumiwa kutibu maambukizi ya virusi vya homa ya nyani.

Dawa fulani za kuua virusi zinaweza kupendekezwa kwa watu walio na uwezekano zaidi wa kuwa wagonjwa sana, kama vile wale walio na mifumo dhaifu ya kingamaradhi. Zungumza na mtoa huduma wako wa afya kuhusu machaguo ya dawa za kuua virusi yanayoweza kukufaa.

Mtoa huduma wako wa afya anaweza kupendekeza aina zingine za matibabu kulingana na dalili zako.

WALINDE WENGINE WALIO KARIBU NAWE

- Jitenge nyumbani wakati wa ugonjwa wako
- Ikiwa una vipetele ambavyo havijapona au dalili zingine, kaa katika chumba tofauti mbali na watu au wanyama vipenzi unaoishi nao, inapowezekana
- Epuka kufanya mapenzi na mtu yeyote hadi vipetele hivyo vikipona, vigaga kuisha na kuwa na safu mpya ya ngozi

KIPINDI CHA KUAMBUKIZA

Homa ya nyani inaweza kuenezwa kuanzia wakati ambapo dalili zitaanza hadi vipetele vikipona, vigaga vyote kuisha na safu mpya ya ngozi kumea.

Ugonjwa huo kwa kawaida hudumu kwa wiki 2-4.



Ikiwa dalili zako zitakuwa mbaya zaidi, wasiliana na mtoa huduma wako wa afya kwa matibabu zaidi.